# TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR

ZBS ZANZIBAR BUREAU OF STANDARDS

ISO 9001: 2015 Certified

TOLEO LA 4




# ZBS KATIKA UFANISI WAKE

VIWANGO. UBORA. MAISHA

Design by: 0718366229

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 1 | Salamu za Rais wa Zanzibar na Serekali ya Mapinduzi | 3 |
| 2 | Salamu za Mhe. Waziri wa Biashara Maendeleo ya Viwanda - Zanzibar. | 4 |
| 3 | Salamu za Mkurugenzi Mkuu wa ZBS | 5 |
| 4 | Mafanikio ya ZBS tokea kuanzishwa | 6 |
| 5 | Kurahisisha upatikanaji huduma za ZBS kupitia mifumo ya iSQMT | 12 |
| 6 | Teknolojia ya ukaguzi wa vyombo vya moto | 14 |
| 7 | ZBS yamaliza kilio cha ubora kwa vifaa vya ujenzi | 16 |
| 8 | Kupokea malalamiko: mwongozo wa mchakato wa kisheria | 18 |
| 9 | Ushiriki wa ZBS katika Maonesho ya Sabasaba | 20 |
| 10 | STC yatoa uelewa juu ya bidhaa hafifu | 22 |
| 11 | Taratibu za ukaguzi wa bidhaa | 24 |
| 12 | Zanzibar kuandaa mkutano mkuu wa ARSO, Juni 2025 | 25 |
| 12 | Tuonavyo sisi | 28 |
| 13 | Tunajivunia kuwa wachangiaji katika kufanikisha miradi ya maendeleo ya ZBS | 30 |
| 14 | Matukio katika picha | 32 |

# SALAMU ZA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI



**Matumizi ya viwango bora vya vyakula, vinywaji na bidhaa nyengine ni muhimu kwa usalama wa jamii na taifa na ni moja ya njia inayosaidia kujenga taifa lenye watu wenye afya nzuri na kujiepusha na athari na hatari mbali mbali katika shughuli zetu za kila siku.**

Kutokana na sababu hio ndio maana Serikali ya Mapnduzi Zanizbar ilianzisha ZBS mwaka 2011 na sasa inaendelea kwa kasi kuimarisha ZBS ili kuhakikisha, kusimamia na kufuatilia viwango vya ubora vinazingatiwa kikamilifu na kwa uadilifu katika sekta zote.

Hii sio tu inasaidia na kuhakikisha usalama wa watu, bali pia inashajihiisha ushindani wenye tija wa bidhaa na huduma zinazotolewa na Zanzibar katika soko la nchi jirani na kimataifa.

Mpaka hivi karibuni, Zanzibar haikuwa na utaratibu madhubuti wa usimamizi wa viwango vya bidha mbalimbali zinazozalishwa nchini na zinazotoka nje.

Lakini sasa tunayo ZBS kama wakala wa serikali na umma katika kuhakisha kila bidhaa inakuwa ni ya kiwango kizuri na salama na kinakubalika kimataifa na hivyo kutopata pingamizi katika soko la kimataifa.

Hii ndio iliopelekea kila kukicha Serikali kuiimarisha ZBS ili kuwa na uwezo na nyenzo za kuboresha viwango nchini. Tunawapongeza kwa juhudi zenu sa kufikia maelengo tuliokusudia katika kuhakikisha Zanzibar inazidi kuwa mfano wa kuigwa katika usimamizi wa kuwa na viwango bora na salama vya bidhaa.

Serikali itaendelea kushirikiana na ZBS na kufanya kila iwezalo kuiimarisha ili iweze kuboresha huduma kwa manufaa ya wananchi wetu. Hii ni kazi muhimu na tunatarajia kuendelea kufanya kazi pamoja kufikia malengo yetu.

Tukumbuke kUfanya kazi kwa bidii, uaminifu na uadilifu ndio chachu ya kujipatia maendeleo yenye tija kwa jamii na nchi. Tushirikiane kuifanya kazi hio kwa pamoja.

**KILA LA KHEIR**

**NAWATAKIA ZBS KILA LA KHERI NA MAFANIKIO KATIKA KUSIMAMIA UWEPO NA MATUMIZI YA WIANGO BORA ZANZIBAR.**

# SALAMU ZA MHE. WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA - ZANZIBAR



ZBS ina wajibu wa kutekeleza jukumu muhimu la kudhibiti na kuboresha viwango vya bidhaa na huduma kwani hilo ni jambo ambalo ni msingi katika kujipatia maendeleo ya biashara na ustawi wa kiuchumi wa Zanzibar.

Nimeridhika na kufurahia kazi nzuri mnayoifanya na kuwaomba muongeze juhudi ili tupate mafaniki makubwa zaidi kwa kuhakikisha bidhaa na huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vya kimataifa tulivyoviridhia na huku kila mfanyakazi kuongeza ushindani wenye manufa.

Hii sio tu itasaidia kulinda usalama wa watu wetu na wanaotembelea nchi yetu, bali pia itaongeza imani ya wateja kwa ZBS.
Ninawapongeza kwa jitihada zenu za utumishi mzuri kwa taasisi na nchi na nawaomba kuendelea na moyo huo kufanya kazi kwa uadilifu na ufanisi.
Ni matumaini yangu mtadumisha na kukiongeza kiwango cha juu cha kazi mliofikia na kuendelea kubuni mikakati na mipango yenye gharama nafuu na isiokuwa na utata ya kuhakikisha viwango vya ubora vinakua na kuboreka.

Tunatarajia kuendelea kuimarisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar ili kufanikisha malengo yetu ya pamoja katika kuendeleza biashara na uchumi wa nchi yetu. Kila la kheri kwa wafanyakazi wa ZBS na wateja wake.

**Maendeleo ya biashara ni viwango.**



## SALAMU ZA MKURUGENZI MKUU WA ZBS

Jarida hili limelenga kutoa taarifa muhimu, habari za hivii karibuni, elimu, maelezo ya kina kuhusu viwango na ubora katika sekta mbalimbali na kuwa daraja la kubadilishana mawazo na wateja wetu na jamii.

Lengo letu, kama ilivyoainishwa katika sheria ya kuanzishwa kwake miaka 13 iliyopita ni kuimarisha uelewa kuhusu viwango vya ubora, kuchangia katika kuboresha huduma na bidhaa na kuongeza ushirikiano kati ya taasisi yetu, tasisi kama hii na ndugu zetu wa Tanzania Bara, nchi jirani na kimataifa na wadau wetu wa ndani na nje.


**VIWANGO. UBORA. MAISHA**

ZBS ZANZIBAR BUREAU OF STANDARDS

*ISO 9001: 2015 Certified*

# SAFARI YA ZBS






# MAFANIKIO YA ZBS TOKEA KUANZISHWA

Safari ya ZBS tokea kuanzishwa kwake imepitia hatua mbali mbali na leo kuwa na sura yenye mafaniki na kutoa matumaini ya kuendelea kufikia malengo yaliopelekea kuasisiwa kwake.

Katika safari hii ZBS imekuwa na mipango ya muda mfupi na mrefu na kuwa na mikakati na mipango kazi ambayo imekuwa kila baada ya muda inafanyiwa tathmini ili kuiboresha. Katika utendaji wake wa kazi ZBS inajtahidi kila inavyowezekana kuitekeleza mikakati na maelekzo yanayotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kuweka mazingira bora ya utendaji kazi na utoaji wa huduma.

Katika kipindi cha miaka minne cha uongozi wa serikali ya awamu ya nane wa Rais Hussein Mwinyi, ZBS imejenga miundombinu madhubuti na ya kisasa chini ya usimamizi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

ZBS ilianzishwa kufuatia kutungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa Sheria ya Viwango ya Zanzibar Na. 1 ya mwaka 2011. Chini ya sheria hio, majukumu makuu ya ZBS ni kuandaa na kusimamia ubora wa viwango vya bidhaa na utoaji wa huduma Zanzibar.Bidhaa hizo ni zile zinazozalishwa nchini au kuingizwa kutoka nje kwa ajili ya kulinda uslama na afya kwa watumiaji wa bidhaa na wanaopata huduma mbali bali, kuhifadhi mazingira ya visiwa vyetu na kushajihisha ukuaji wa uchumi.

## Majukumu Makuu ya ZBS.

Taasisi hii pia ina jukumu la kuendeleza na kukuza viwango vya bidhaa, uthibitishaji, usimamizi ubora kupitia ukaguzi katika maeneo ya uzalishaji na kwenye soko na kufanya upimaji wa kitaalamu wa bidhaa kwa kutumia vifaa vya maabara kwa mujibu wa matakwa ya viwango husika.

Hali hii itapelekea kukuza na kujenga imani kwa wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji.Vievile itachangia kuimarisha

uchumi wa Zanzibar na kulinda afya na usalama wa jamii ya watu wa Visiwani na wale wanaotumia bidhaa hizo nje ya nchi.

## Njia na takwimu ya uwepo wa viwango ZBS.

Uandaaji wa Viwango vya Zanzibar hufanywa kupitia mchakato wa mashauriano ambapo hatimaye huwekwa muongozo, mfumo na kanuni za upimaji wa viwango vinavyokubalika kikanda na kimataifa. Kazi hii ya kuweka vipimo vya viwango hufanywa na kamati za ufundi kwa bidhaa husika.

Kamati hizi zinaundwa na wataalamu wanaowakilisha wadau anuwai ili kuhakikisha kunakuwa na uwakilishi wa usawa. Hadi kufikia mwezi wa Januari 2025, ZBS imeandaaa viwango 692 ambavyo baadaye viliidhinishwa ili kufikia malengo ya kuwa na viwango vinavyoendana na bidhaa zinazotumika kwa lengo la kusimamia ubora wa bidhaa hizo. miongoni mwa viwango hivyo ni vya chakula, uhandisi mitambo , vifaa vya ujenzi, kemikali, umeme, mazingira na huduma ya utalii .

Halikadhalika, viwango 33 viko katika taratibu za kusainiwab na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda ili vianze kutumika. Hatua hii ya kuvithaminisha viwango huenda sambamba na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.




## Uboreshaji wa upimaji wa bidhaa

Katika awamu hii ya aane ya uongozi wa Dk. Mwinyi Taasisi imepata vifaa vipya na vya kisasa vya maabara ili kuhakikisha upimaji wa bidhaa unatekelezwa kwa ufanisi. Hivi sasa bidhaa nyingi zaidi, zikiwemo za kemia ya chakula, kielektroniki na umeme na mafuta ya nishati zinapimwa na ZBS. Upimaji wa sampuli za bidhaa ni hatua muhimu sana katika kusimamia viwango na kudhibiti ubora wa bidhaa.

## Maendeleo ya maabara ya chakula.

Maabara hii imefungwa vifaa vya kisasa vyenye uwezo mkubwa, ikiwemo Gas Chromatography (GC), kifaa ambacho hutumika kuchambua mchanganyiko wa kemikali katika sampuli.

Katika GC, sampuli huingizwa kwenye kipande cha gesi, ambapo inachujwa kupitia safu ya gesi (koloni) ambayo ina vifaa maalum. Aina tofauti za kemikali katika sampuli hugawanyika kwa sababu ya tofauti zao katika uhamaji kupitia koloni. Hii husaidia kutambua na kuhesabu viwango vya kemikali mbalimbali zilizomo katika sampuli hiyo. GC ni muhimu katika tasnia nyingi, ikiwa ni pamoja na kemia, dawa, na mazingira. na Atomic Absorption Spectroscopy (AAS).

AAS ni mbinu ya uchambuzi inayotumiwa kupima viwango vya vipengele fulani katika sampuli. Inategemea kanuni ya kwamba atomi za elementi hizo zinaweza kunyonya mwangaza wa mawimbi fulani. Katika mchakato huu, sampuli inachomwa ili kubadilishwa kuwa gesi, kisha mwangaza wa mawimbi maalum hupitishwa kupitia gesi hiyo. Wakati atomi zinanasa mwangaza, kiasi cha mwangaza kinachonyonywa kinatumika kubaini mkusanyiko wa elementi husika. AAS ni muhimu katika uchambuzi wa mazingira, afya na viwanda.



## Uwezo wa maabara ya umeme

Maabara hii ina uwezo wa kupima vifaa vya umeme na elektroniki vinavyotumika majumbani, kama pasi, chombo cha kuchanganya vitu (blendor), Feni, tanuri (Oven) na chombo cha kupikia chakula "Rice cooker".



## Uimarishaji wa maabara ya kupimia mafuta ya nishati na vilainishi vya mafuta

Maabara hii ina uwezo wa kupima aina zote za mafuta ya nishati yanayoingizwa nchini, zikiwemo mafuta ya ndege, mafuta ya taa, dizeli na petroli. Aidha, maabara hii ina uwezo wa kupima vilainishi vya mafuta ya aina zote.



## Maabara ya uhandisi ujenzi.

Hii ni maabara inayotumika kupimia vifaa vya ujenzi, kama saruji, nondo, lami, udongo, vigae (tiles) n.k ili kuleta ufanisi wa kuhakiki kupata bidhaa bora za ujenzi zitazosaidia kuhakikisha kuwa na majengo salama.



## Maabara ya nguo na ngozi

Maabara hii inapima bidhaa za nguo na ngozi kama vile kanga, vitenge, mashuka na aina nyengine za nguo. Vilevile itatumika kupima bidhaa nyengine zinavyotengenezwa kwa ngozi kama viatu, mikoba na mikanda.
Miongoni mwa vigezo vitakavyotumika katika kuzipima bidhaa hizo ni uzito katika sarafu( grammes) ya bidhaa , kasi ya rangi, kiwango cha asidi (pH value), kiwango cha kupungua au kurefusha, nguvu ya mkazo na kuvunjika kwa bidhaa.

## Maabara ya vifungashio

Maabara hii itapima vifungashio vya bidhaa mbalimbali na itawasaidia wenye viwanda na wajasiriamali kuwa na vifungashio venye viwango vya juu.



## Maabara ya chakula na vimelea

Maabara ya chakula vimelea au kwa jina la kitaalamu 'Microbilojia' ni yenye sayansi ya utafiti wa viumbe vidogo kama, bakteria visivyo onekana kwa macho moja kwa moja, bali kwa kutumia hadubini (microscope).Viumbe hivi vidogo (micro-organism) vinaweza kuishi sehemu yoyote Ulimwenguni, licha ya kuwa na madhara wakati mwingine na pia huwa uwepo wake ni muhimu kulingana na mazingira husika.
Maabara hii pia ina uwezo wa kupima sampuli kwa kutumia maikrobaiolojia (micro bio challenge test) ili kuua vimelea au wadudu waliokusudiwa.ZBS inajivunia uwepo wa maabara hii kwani kusaidia kuhakikisha bidhaa zote za aina hii zipo salama kutumika.



## Maabara ya ugezi

Hii ni mabara ya ugezi ina uwezo wa kulinganisha kwa kufanya uhakiki wa usahihi wa vipimo mbali mbali ili kufanya ugezi wa vipimo vyote ambavyo vinatumika katika uzalishaji viwandani na kwenye hospitali.

ZBS imepokea mradi wa BIG-Z unaosimamiwa na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Mradi huu ni mpango maalum wa uimarishaji wa huduma za ZBS katika upatikanaji wa vifaa vya maabara na tayari ZBS imeshapatiwa vifaa vya maabara ya ujenzi. Maabara hizi zinauwezo mkubwa wa kupima sampuli mbalimbali na kufanya uchunguzi wa kimaabara, na kuhakikisha kuwa zimekidhi vigezo vilivyowekwa.

Matumizi ya maabara hizi inapelekea kuwepo ufanisi mzuri na wa haraka katika kupata majibu ya sampuli zinazoingizwa au zinazozalishwa na kupunguza changamoto ya uchelewaji wa majibu ya maabara kwa sampuli husika.

Uwezo wa maabara hizi umepelekea kuwa na mashirikiano makubwa na taasisi kadhaa zinazo simamia uingizaji wa mafuta nchini uliopelekea Zanzibar kwa sasa kupokea mafuta yaliyo salama na ambayo hayajachakachuliwa.





## Kituo cha ukaguzi wa magari na vyombo vya moto

Jukumu jengine muhimu la ZBS ni kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini zina ubora unaohitajika. Hii inajumuisha bidhaa za vyombo vya moto kama magari, honda, bajaji , guta n.k.

Katika juhudi zake za kutekeleza wajibu huu kwa ufanisi ZBS inacho kituo kikubwa na cha kisasa cha ukaguzi wa vyombo vya moto kitakachokua na vifaa vya kisasa. Mradi huu wa vyombo vya moto unaosimamiwa na ZBS umegawanyikas ehemu tatu:

**i.** Sehemu ya kukagua vyombo vya moto.
**ii.** Sehemu ya ofisi na
**iii.** Sehemu ya kazi za nje.



Baada ya kukamilika kwa mradi huu wa ukaguzi wa magari eneo hili lina uwezo wa kukagua zaidi ya magari 300 kwa siku. Aidha, katika eneo hili taasisi ambazo zitajumuika katika utoaji wa huduma hizi ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa utoaji wa vibati, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa malipo, Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kwa malipo ya bima za vyombo vya moto pamoja na Mamlaka ya Usafirishaji na Leseni Zanzibar (ZARTSA)

Utekelezaji wa mradi huu mkubwa ni miongoni mwa mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa Dk. Mwinyi. Matarajio makubwa katika kituo hiki ni;-

**i** kuwa kituo nambari moja cha kisasa nchini katika upimaji vyombo vya moto kwa kuwa na mashine na mitambo ya kidigitali

**ii** Kituo hiki kitaondoa changamoto ya urasimu na usumbufu katika utoaji wa huduma ya upasishaji wa vyombo vya moto kwa kuwa huduma zote muhimu zitatolewa katika eneo moja. Vile vile kitaongeza uwezo na ufanisi katika ukaguzi wa vyombo vya moto na kuhakikisha kuwepo na usalama wa matumizi ya vyombo hivyo.

**iii** Kitaongeza pato la Taasisi na Serikali kwa ujumla kwa kupitia ukaguzi wa vyombo vingi zaidi kwa siku moja.



## Uimarishaji wa mifumo ya ndani ya Taasisi.

Kukamilika kwa mradi huu ni mafanikio makubwa ya awamu hii ya uongozi wa Rais Mwinyi kwa vile utasaidia sana kuhakikisha ufanisi wa utoaji huduma za ZBS. Mradi umeboresha huduma na kupelekea kuondoa mlolongo na usumbufu wa upatikanaji wa huduma mbalimbali, kama utoaji wa leseni, alama ya ubora au upimaji. Vile vile mradi hu unaojulikana kwa jina la iSQMT unatoa tathmini halisi ambayo itawaridhisha wateja wake unadhaminiwa na trademark Africa (TMEA).

## Uhamasishaji wa upatikanaji alama ya ubora

Katika kuhakikisha wajasiriamali wanaweza kuwa na bidhaa zenye alama ya ubora na kuweza kufanikiwa kuingiza sokoni bidhaa zilizo bora ZBS ilichukua jukumu la kuandaa taratibu,miongozo ya kisheria na kanuni zilizowezesha kuweka mpango kazi wa mwaka.Hii itawasaidia wajasiriamali kupata alama ya ubora Wajasiriamali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika utekelezaji wa mpango huu ZBS inayo Hati ya Maelewano (Memorundum of Understanding –MOU) na Wakala wa uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) ili kuweka miundo mbinu muhimu ya upatikanaji wa alama ya ubora.




## ZBS na uingizaji wa bidhaa nchini.

ZBS imefanikiwa kufanya mabadiliko makubwa katika uingizaji wa bidhaa nchini kwa kutumia mfumo wa PVoC (kukagua bidhaa nje ya nchi) na DI (ukaguzi wa ndani wa bidhaa) kupitia maabara zake.

Katika kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na zinazoingia nchini ZBS imezingatia viwango na ubora katika nchi yetu na kutoa zaidi ya leseni 100 za alama ya ubora kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na nje.

ZBS inajivunia hatua hii kwani itaondoa kilio cha wenye viwanda na wajasiriamali na kuwawezesha kufikia malengo ya bidhaa zote zinazozalishwa nchini kuwa na ubora kwa kutumia alama ya ubora ya ZBS.




## Uimarishaji wa majengo ya Taasisi

Upatikanaji wa jengo la maabara na ofisi katika eneo la Maruhubi ni moja kati ya maendeleo ya uboreshaji wa shughuli za usimamizi wa viwango za ZBS. Z

BS imefurahia uamuzi wa Serikali ya awamu hii ya nane kuipatia eneo maalum la ekari 12 liliopo mbele ya makao makuu ya ofisi za ZBS. Eneo hili hivi sasa linafanyiwa ukarabati mkubwa na kujengwa maghala maalum kwa ajili ya uhifadhi wa bidhaa zinazopimwa. Vile vile katika eneo hili panajengwa maabara maalum ya metrolojia na kupanuliwa maabara ya kemia itakayosimaia upimaji wa vilainishi.



## Ujenzi wa ofisi za ZBS Pemba.

ZBS hivi sasa imekamilisha mpango wa ujenzi katika ofisi yake ya Pemba katika eneo la Chamanangwe, Chake Chake.
Hata hivyo Ofisi ya Pemba hivi sasa ina mazingira mazuri ya kiutendaji na inatoa baadhi ya huduma za msingi, kama kufanya ukaguzi wa sampuli, upimaji wa bidhaa zinazozalishwa ndani, viwandani na kilimo kwa lengo la kuzuia ungizaji nchini kwa bidhaa zilizo chini ya viwango.Hapo kabla kazi hii ilikuwa inafanyika katika mabara za ZBS ziliopo Unguja



## Kukubalika katika utendaji kikanda na kimataifa

Miongoni mwa mafankio ambayo ZBS inafurahia ni kufikia viwango vya kimataifa kupitia ushirikiano na mashirika ya viwango ya kimataifa ,kama Shirika la Viwango Afrika (ARSO). Hatua hii imechochea maendeleo ya haraka kwa taasisi.



## Uimarishaji wa Sheria na Kanuni.

Taasisi imeandaa na kupitia sheria kwa lengo la kuimarisha na kuanzisha kanuni mpya ili kuondoa mapungufu katika utekelezaji wa majukumu ya ZBS kwa lengo la kuimarisha huduma za upatikanaji wa viwango vya ubora na uhakiki wa usalama wa bidhaa.

## Elimu na Uhamasishaji.

Elimu ni muhimu sana katika kazi yoyote ile, ikiwa pamoja na biashara. Kutokana na umuhimu huu ili wajasiriamali na wafanya biashara wapate mafanikio ZBS imeweka mipango maalum ya uelimishaji umma na sekta binafsi juu ya umuhimu wa viwango vya ubora.
Chini ya mpango huu zipo programu mbali mbali za mafunzo, warsha na mikutano ya kuhamasisha matumizi bora ya viwango.Hii inaenda sambamba na kushirikisha sekta binafsi, vyuo vikuu na mashirika ya kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha wadau wake wana uelewa juu ya viwango,elimu inayotolewa inaakisi mabadiliko ya mahitaji ya soko na maendeleo sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia.



## Tuzo na Heshima.

Taasisi katika kipindi kifupi imepata tuzo na heshima baada ya kuwa na program yake kuu ya ushiriki katika kutoa misaada ya kijamii na kuchangia mikutano ya kimaendeleo katika taasisi mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma yake inayoitoa ya viwango vya ubora, jambo ambalo linathibitisha kufanikiwa kwa jitihada zake za kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya viwango.



## Utendaji kazi kiufanisi .

ZBS imepunguza udanganyifu na kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa katika sekta ya biashara kwa kuboresha mifumo ya usimamizi na udhibiti wa viwango na kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zina ubora wa hali ya juu.

# KURAHISISHA UPATIKANAJI HUDUMA ZA ZBS KUPITIA MIFUMO YA ISQMT




ZBS imepanua huduma zake ili kufikia malengo ya utoaji huduma sahihi, bora na kwa wakati. Katika kuitekeleza kazi hii ZBS imeweka njia ya uanzishaji wa upatikanaji bora wa huduma kwa maeneo yaliyopo na mapya katika sekta mbali mbali.Hii ni pamoja na kuanzisha huduma za mtandaoni na mifumo ya habari ili kuwarahisishia wadau kupata taarifa na huduma kwa ufanisi.

Mafanikio haya yanaonyesha maendeleo makubwa katika kuboresha viwango na kuimarisha hali ya biashara na huduma za Zanzibar na yanaweka misingi mizuri kwa ukuaji zaidi katika siku zijazo. Kurahisisha upatikanaji wa huduma za ZBS kupitia mifumo ya ISQMT (Integrated Standards and Quality Management Technology) inaweza kufanywa kwa hatua zifuatazo:

**Kujenga Mfumo wa Kidijitali:**


Kuunda jukwaa la mtandaoni litatumiwa na wateja, wafanya biashara na wadau wengine kupata huduma za ZBS kwa urahisi.Hii inajumuisha mambo mengi, ikiwa pamoja na usajili, uwasilishaji wa maombi na kupokea taarifa za huduma.

**Taarifa za moja kwa moja za huduma:**


Kuanzisha mifumo ya moja kwa moja inayowezesha wateja kupata taarifa kuhusu maombi yao, viwango vya ubora, na upya wa vyeti bila kuhitaji kufika ofisi au kuwasiliana moja kwa moja na ofisi.

**Uboreshaji huduma ya maalalamiko na ushauri:**


ZBS imeweka mfumo wa kidijitali wa kupokea na kusimamia malalamiko, mapendekezo na ushauri kutoka kwa wateja.Mfumo huu unakusudiwa kusaidia , kuhakikisha matatizo wanayokutana nayo wateja yanashughulikiwa kwa haraka na kwa ufanisi.




**Teknolojia ya Takwimu (Data):**
Mfumo huu umeweza kuweka hifadhi teknolojia ya takwimu unayowezesha kutunza na kupokea taarifa za maombi, rekodi za ukaguzi na taarifa nyingine muhimu kwa matumizi ya ZBS na wadau.




**kutoa Huduma za Mtandao:**
Huduma hii ya mtandao ni ya maelezo ya viwango, mwongozo wa usajili na nyaraka zinazohitajika kwa njia rahisi na haraka.



**Uwekaji wa Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini:**
Mfumo huu umeanzishwa ili kufuatilia utoaji wa huduma na tathmini ya kuridhika kwa wateja kupitia tafiti na maoni na kuweza kuboreshwa kwa huduma kulingana na matokeo ya tathmini.



**Huduma ya Msaada kwa Wateja:**
Baadhi ya wakati wateja hutaka msaada ili kupata huduma zinazotolewa na Taasisi. kwa lengo la kutimiza haja hio , ZBS imeweka mfumo wa msaada kwa wateja kwa kuwa na dawati maalum la kuifanua kazi hio (helpdesk). Katika mfumo huu dawati linajibu masuali yanayoulizwa mara kwa mara pia linazungumza moja kwa moja na wadau, kutoa ushauri na taarifa za haraka juu ya huduma za ZBS.



**Mafunzo na Uhamasishaji:**
Uhamasishaji una taaluma na mbinu zake za kufanya kazi hii. Kwa kuelewa hili, ZBS inatoa mafunzo kwa wateja na wafanyakazi wake juu ya matumizi ya mifumo ya ISQMT ili kuhakikisha panakuwepo matumizi ya ufanisi na kuongeza uwazi katika huduma zinazotolewa. Kupitia hatua hizi, ZBS imeboresha upatikanaji wa huduma zake, imeongeza ufanisi na imerahisisha uzoefu wa wateja kwa kutumia teknolojia ya kisasa.





# TEKNOLOJIA YA UKAGUZI WA VYOMBO VYA MOTO

ZBS imejenga kituo cha kisasa chenye kutumia teknolojia ya kisasa kukagua vyombo vya moto kiliopo Maruhubi.
Kituo hichi kina lengo la kuimarisha ubora wa vyombo vya moto vinavyoingizwa nchini, sambamba na hili kituo hichi kimejumuisha kituo jumuishi cha pamoja kinachotoa huduma kwa wamiliki wa vyombo vya moto ili kurahisisha taratibu za upatikanaji wa mahitaji ya vyombo hivyo ,kama vile usajili ,ambao unapatikana kupitia ZRA pamoja na kupata bima za vyombo hivyo kutoka ZIC.
Aidha katika kituo hicho taratibu za malipo zote hufanyika katika ofisi ya PBZ.

**i. Uanzishaji wa Mfumo wa Kidijitali:**
Ukaguzi wa vyombo vya moto unaofanyika kwa kutumia mitambo ya ukaguzi ambayo imeunganishwa na mfumo maalum wa kidijitali unaotumika kutuma taarifa za vigezo vyote vya ubora na usalama wa vyombo hivyo kwa mujibu wa matakwa ya viwango husika. Kuanzishwa kwa mfumo huu umepelekea kufanyika kwa kazi za kuwasilisha, kufuatilia na kupokea ripoti za ukaguzi wa vyombo vya moto kupitia katika mfumo.
Aidha ZBS inatarajia kuainisha mfumo wake huo na mifumo wa ZRA ili kuwa na mfumo wa Dirisha la pamoja ambapo kwa kiasi kikubwa utarahisisha mawasiliano kati ya ZBS, ZRA, TRA na wateja.

**ii. Usimamizi wa Taarifa kwa Pamoja:**
Mfumo wa usimamizi wa taarifa ambao utakuwa na taarifa za vyombo vya moto pindi vinapoingizwa nchini utahusisha taarifa za chombo husika, taarifa za ukaguzi pamoja na taarifa za usajili wa vyombo hivyo vya moto hivyo utasaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wake wakati wowote kuwa rahisi.

**iii. Mchakato wa Uidhinishaji wa Kumbukumbu:**
Mchakato huu unarahisisha taratibu za uidhinishaji wa vyeti vya ukaguzi wa vyombo vya moto kwa kushirikiana kwa karibu na ZRA. Hali hii inapunguza muda wa kusubiri na kuongeza ufanisi katika kupata huduma nyengine, kama vile bima za vyombo vya moto.

**iv. Huduma za Mteja Mtandaoni:**
Huu ni mfumo wa utoaji wa huduma kwa mteja kupitia mtandaoni, kama kufuatilia maombi ya ukaguzi, kutuma maombi kwa

ajili ya usajili wa vyombo vya moto na kupokea taarifa kuhusu hali ya vyombo vyao. Hii inaengeza ufanisi katika utendaji na kupunguza urasimu kwa wateja.

**v. Kuweka Viwango vya Pamoja:**
Jukumu la ZBS ni kuweka viwango , utaratibu huu hufanyika kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali, wakiwemo watumiaji wa vyombo vya moto ambao kwa namna moja au nyengine wanaweza kusaidia kuweka miongozo na viwango kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

**vi. Mafunzo na Uwezeshaji:**
Kila kazi huwa na mabadiliko na ili kuenda sambamba na mabadiliko yanayotokea. ZBS inatoa mafunzo ya ukaguzi kwa wakaguzi w. Mafunzo hayo husaidia kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vya juu na zinakubaliana na sheria zilizopo.

**vii. Uwekezaji katika Teknolojia:**
ZBS inatumia teknolojia ya kisasa katika vituo vya ukaguzi ili kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa vyombo vya moto.

**viii. Kurahisisha Taratibu za Uwasilishaji:**
Katika kuhakikisha inapunguza vikwazo katika taratibu za uwasilishaji wa vyeti vya ukaguzi, ZBS imeandaa mifumo rahisi na yenye ufanisi. Mifumo hii inafanyiwa tathmini kila baada ya muda kwa lengo la kuiboresha zaidi.

**ix. Kufanya Utafiti na Tathmini:**
Lengo la kuanzisha mifumo ya tathmini na ufuatiliaji ni kupima ufanisi wa huduma na kubaini maeneo ya kuboresha katika mchakato wa ukaguzi.
Kupitia hatua hizi, mashirikiano kati ya wakaguzi wa vyombo vya moto na ZRA yataimarishwa na huduma zitapatikana kwa rahisi na za haraka kwa wateja.

## KITUO JUMUISHI











# ZBS YAMALIZA KILIO CHA UBORA KWA VIFAA VYA UJENZI

ZBS hivi karibuni ilituliza kilio cha muda mrefu cha waingizaji na wenye viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za ujenzi kufuatia kuwekwa kwa maabara ya upimaji wa vifaa vya ujenzi (uhandisi ujenzi)".

Hatua hii imeleta mabadiliko makubwa ya kupelekea kuwepo viwango vyenye ubora wa daraja la juu na kuondoa athari na hatari za kuwa na viwango duni katika soko la vifaa vya ujenzi.

Hivi sasa utaratibu wa ukaguzi wa upimaji wa bidhaa za ujenzi ulioanzishwa na ZBS unahakikisha vifaa vya ujenzi vinavyouzwa na kutumika katika miradi ya ujenzi vina viwango vya juu vya ubora.Sera ya ZBS imetoa umuhimu katika kuhakikisha vifaa vya ujenzi vinakidhi mahitaji maalum ili kuepuka athari za kuwa na majengo na miundo mbinu dhaifu ambayo itahatarisha usalama.

**Faida za kuwa na maabara ya vifaa vya ujenzi**

Kuwepo kwa maabara hii kuna faida nyingi na miongoini mwao ni :-

i. **Mabadiliko ya Teknolojia:** Kwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia ambayo yameweka pembeni vifaa vya zamani na kuweka mazingira mazuri ya kutumia vifaa vya kisasa bila ya matatizo.

ii. **Kupunguza Gharama:** Kutotumia vifaa zamani kunasaidia kupunguza gharama za uzalishaji na ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

iii. **Kuboresha upatikanaji wa huduma:** Kuondoa vikwazo vya zamani vya uingizaji wa bidhaa na kufanya upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya ujenzi na hatimaye kuharakisha kazi za ujenzi.

iv. **Ubora wa viwango unapokuwa wa chini:** Kama viwango vya ubora sio vya juu panakuwepo mwanya wa kuingiza sokoni vifaa vya chini ya kiwango, jambo ambalo linaathiri ubora wa majengo na miundombinu.

**v. Matatizo ya Usalama:** Vifaa vya ujenzi vya chini ya kiwango vinaongeza hatari za usalama katika miradi ya ujenzi.

Kwa kuwa ZBS imefuta kilio hiki ni muhimu kwa wadau wa sekta ya ujenzi kuwa makini na kuendelea kufuatilia viwango vya ubora vilivyoainishwa na mashirika mengine au vyanzo vya kimataifa. Wadau wanaweza kushirikiana na ZBS ili kuhakikisha vifaa vinavyotumika vina ubora wa kutosha na vipo salama kwa matumizi. Hatua hii ya ZBS inapaswa kusimamiwa kwa umakini ili kuhakikisha sekta ya ujenzi inabaki salama na yenye ufanisi.


## VIFAA VYA KISASA VYA MAABARA YA UJENZI


















ZBS ZANZIBAR

ZANZIBAR BUREAU OF STANDARDS

PROCEDURE FOR HANDLING COMPLAINT

ZBS CONTROLLED COPY

ZBS/PRM/PR-01
Vn 03 of 2024

# KUPOKEA MALALAMIKO: MWONGOZO WA MCHAKATO WA KISHERIA

Kusikiliza malalamiko ni muhimu katika usimamizi wa huduma, upatikanaji wa haki na kuwepo uhusiano mzuri na maelewano. Taratibu za upokeaji malalamiko zinaweza kutofautiana kulingana na aina ya shirika au kiwanda, lakini madhumuni ni kuhakikisha masuala yanayoibuka yanashughulikiwa kwa njia ya haki na ya kitaaluma.

Ufuatao hapa chini ni mwongozo wa jinsi ya kufuata taratibu hizi kwa ufanisi:
Uelewa wa mfumo wa malalamiko kwa mtazamo wa mfumo wa usimamizi ubora wa ZBS "QMS".

Taratibu maalum zilizopitishwa katika mfumo wa usimamizi ubora ni muhimu kwani zimewekwa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji na matokeo mazuri ya majibu ya malalamiko yaliyowasilishwa.

Kabla ya kuwasilisha malalamiko ni muhimu kuelewa mfumo na taratibu zinazotumika. Mfumo wa malalamiko mara nyingi unajumuisha hatua zifuatazo:

i. **Kupokea malalamiko:** Kwa kawaida, malalamiko huwasilishwa kwa njia ya maandiko, barua pepe au simu. Baadhi ya mashirika yana fomu maalum za malalamiko.

ii. **Kuhakiki malalamiko:** Mara baada ya kupokelewa malalamiko hupitiwa ili kubaini uhalali na uharaka wa suala hilo.

iii. **Kuchunguza malalamiko:** Uchunguzi hufanywa ili kujua ukweli wa malalamiko na kutathmini hatari au madhara yanayoweza kutokea.

iv. **Kutoa majibu:** Baada ya uchunguzi, majibu hutolewa na hatua za kurekebisha au kufidia kuchukuliwa.

**Hatua za kupokea malalamiko**
Mteja aanatakiwa kueleza lalamiko lake kwa uwazi kama ifuatavyo;-
Kuandika malalamiko yake kwa uwazi, kueleza kwa kina tatizo alilokutana nalo. Ni muhimu kuzingatia matumizi ya lugha ya heshima na isiokuwa na maelezo au maneno yenye utata.

**Taarifa muhimu:**
Mteja anatakiwa kuhakikisha anajumuisha maelezo muhimu kama tarehe, mahali tatizo lilipotokea, majina ya watu anaowona kuwa ndio waliohusika na nyaraka zinazohusiana na suala hilo.

**Jinsi ya kuwasilisha malalamiko:**
Mteja atatakiwa kuwasilisha taarifa sahihi

kwa kupitia njia ziliyoainishwa na taaisisi ya viwango. Nazo ni barua pepe maalum au kupitia mfumo wa mtandaoni.

**Uhifadhi wa nakala:** Mlalamikaji anatakiwa kuhifadhi nakala ya malalamiko, pamoja na uthibitisho wa upokeaji ili kuweza kufuatilia mchakato wa upatikanaji majibu kwa malalamiko yaliyofuata utaratibu uliowekwa na mfumo wa usimamizi ubora.

**Kufuatilia malalamiko:**
Mteja atatakiwa kufuatilia lalamiko lake ikiwa hajapokea mrejesho ndani ya muda unaotarajiwa kujibiwa ambao ni siku tano. Kwa mujibu wa mkataba wa huduma inapendekezwa baada ya uwasilishaji wa malalamiko mteja atatatakiwa kuwasiliana na ofisi husika ili kujua suala hilo limefikia wapi. Afisa muhusika aliekabidhiwa dhamana ya usimamizi wa ufuatiliaji wa hayo malalamiko atatakiwa kuwa na anuani ya mlalamikaji ili aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi katika kumpatia majibu.Kusikiliza na kufuatilia lalamiko la mteja ni muhimu kwa maendeleo ya taaisisi katika kumridhisha mteja na kuwa na ufanisi wa kazi.

**Hatua za kurekebisha na majibu**
**i. Kupokea Mrejesho:** Baada ya uchunguzi, mteja atapokea mrejesho wa matokeo ya uchunguzi na hatua zilizochukuliwa. Mrejesho huu unaweza kuwa kwa barua rasmi au taarifa ya simu.

**ii. Kukubaliana na hatua:** Kama malalamiko yamethibitishwa, hatua za kurekebisha zitachukuliwa.

**iii. Rufaa:** Ikiwa mteja hajaridhika na majibu au hatua zilizochukuliwa anaweza kuwasilisha rufaa kwa ngazi ya juu au kwa mamlaka nyingine yenye uwezo wa kushughulikia suala hilo.

**Athari za mchakato wa malalamiko:**
Kuweka mfumo mzuri wa malalamiko kunasaidia kuboresha huduma na kujenga uaminifu wa wateja na inasaidia kujua maeneo yenye matatizo na kuweza kuboresha utendaji.
Taratibu za upokeaji wa malalamiko ni muhimu katika kuhakikisha kuwa haki inatendeka na huduma zinaboreka. Kufahamu na kufuata taratibu hizi kunasaidia kutatua matatizo kwa ufanisi na kuimarisha mahusiano kati ya wateja na mashirika. Kwa hivyo, ni muhimu kwa kila mtu kufahamu taratibu hizi na kutekeleza mchakato wa malalamiko kwa usahihi.

**WANANCHI WAKIWASILISHA MALALAMIKO KUPITIA MAONESHO**





# USHIRIKI WA ZBS KATIKA MAONESHO YA SABASABA




Maonesho ya Sabasaba ambayo hufanyika kila mwaka ni jukwaa muhimu la kuonyesha bidhaa, huduma na teknolojia zinazopatikana katika soko la ndani na kimataifa. Tukio hili linaloandaliwa na TANTRADE (Tanzania Trade Development Authority) linatoa fursa kwa mashirika, wajasiriamali na wadau wa biashara kuwasilisha na kuonyesha maendeleo yao. Mwaka huu, ZBS imeshiriki maonesho haya na kuonesha kwa vielelezo mchango wake katika kukuza viwango vya ubora na kuhakikisha usalama wa bidhaa na urahisi wa kuwafikia wadau wake waliopo Tanzania Bara na Visiwani.

**Malengo ya ushiriki wa ZBS**

ZBS, kama taasisi yenye jukumu la kuhakikisha bidhaa na huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vya ubora ilitumia maonesho haya kama fursa ya:

**i. Kujitangaza:** Kuweka wazi majukumu, huduma na mchango wa ZBS katika kuhakikisha ubora wa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini.

**ii. Kuongeza Uelewa kwa wadau :** Kuwafahamisha wadau na umma kuhusu viwango vya ubora, kanuni na taratibu zinazotumika katika usimamizi wa bidhaa.

Kukuza Ushirikiano: Kuimarisha uhusiano na wadau wa biashara, viwanda na mashirika ya kitaifa na kimataifa.

**Maonyesho na Maudhui**

Katika maonesho haya, ZBS ilionesha yafuatayo:

**i. Huduma za Viwango vya Ubora:** Maonyesho yalijumuisha taarifa kuhusu huduma za uthibitishaji wa ubora, maabara na upimaji wa bidhaa.

**ii. Mikakati ya Usimamizi wa Ubora:** ZBS ilielezea mikakati ya kutekeleza viwango vya ubora katika sekta mbalimbali, ikiwa pamoja na ujenzi, kilimo na bidhaa za matumizi ya kila siku.

**iii. Mafunzo na elimu:** Wataalamu wa ZBS walitoa mafunzo na elimu juu ya umuhimu wa viwango vya ubora na jinsi ya kuzingatia kanuni zilizowekwa.

**Athari za ushiriki wa ZBS**

**i. Kukuza uelewa:** Kushiriki kwa ZBS kumeongeza uelewa wa umuhimu wa viwango vya ubora na hivyo kusaidia wajasiriamali na watengenezaji kuboresha bidhaa zao.

**ii. Kuimarisha ubora:** Kwa kushiriki katika maonesho haya, ZBS imeweza kutoa

mwongozo na msaada kwa wajasiriamali na hivyo kuboresha ubora wa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa sokoni.

**iii. Kuongeza ushirikiano:** Ushiriki huu umeiwezesha ZBS kujenga ushirikiano mpya na wadau mbalimbali, ikiwa pamoja na mashirika ya kimataifa na kampuni zinazozalisha bidhaa za kisasa.

**Maoni ya wadau na matokeo:**

Wadau wa maonesho, wajasiriamali, watengenezaji, na wananchi walipongeza juhudi za ZBS za kuleta elimu na mwongozo kuhusu viwango vya ubora.

Watu waliotembelea banda la ZBS walionyesha kuridhika na msaada waliopewa na walisisitiza umuhimu wa kuendelea na ushirikiano wa karibu ili kuhakikisha bidhaa zinazoingia sokoni zinakidhi viwango vya juu vinavyohitajika.

Ushiriki wa ZBS katika maonesho ya Sabasaba umekuza uelewa wa viwango vya ubora na kuboresha huduma za uthibitishaji wa bidhaa. Kwa kuonyesha huduma zake na kutoa elimu kwa wadau, ZBS imeimarisha nafasi yake kama mshirika muhimu katika usimamizi wa ubora wa bidhaa nchini. Ushiriki huu unachangia na kuimarisha soko la bidhaa bora, kuongeza usalama na kuhamasisha maendeleo ya kiuchumi.

## BANDA LA ZBS HUTEMBELEWA NA VIONGOZI MBALIMBALI








# STC YATOA UELEWA JUU YA BIDHAA HAFIFU



Kamati ya Kitaalamu ya Bidhaa Hafifu (STC) ya ZBS ni chombo muhimu katika kuhakikisha ubora na usalama wa bidhaa zinazotolewa sokoni. Kamati hii inajumuisha wataalamu wenye ujuzi katika nyanja mbalimbali, ikiwa ni pamoja na sayansi ya bidhaa, sheria na afya ya umma.

Lengo lake kwa ujumla ni kufuatilia na kutathmini bidhaa hafifu, kubuni viwango vya ubora na kutoa mwongozo kwa wazalishaji. Kwa kazi hii, STC ina jukumu la kusaidia ulinzi wa watumiaji na kuimarisha imani ya watu

Kamati hii imeundwa kwa mujibu wa kanuni ya uthibiti ubora ya mwaka 2014 yenye majukumu yafuatayo:-

**i.** Kuidhinisha vigezo vya bidhaa (Product Specification) vilivyowasilishwa pale ambapo bidhaa ya mzalishaji au mteja amewasilisha vigezo hivyo baada ya ZBS kutokuwa na Kiwango cha bidhaa husika.

**ii.** Kuishauri ZBS jambo lolote lile ambalo linahusiana na vigezo vya bidhaa (Product specification).

**iii.** Kufanya mapitio ya nyaraka zozote zile kwa lengo la kutoa mapendekezo kwa ZBS juu ya taratibu za kufuata au hatua za kuchukuliwa (Ripoti za Ukaguzi, Ripoti za Upimaji wa bidhaa na vigezo vya bidhaa au viwango).

**iv.** Kufuatilia masuala yote yanayohusiana na vigezo vya bidhaa au viwango.

**v.** Kufanya kazi nyengine yoyote ile itakayoagizwa na Mkurugenzi Mkuu ambayo inahusiana na masuala ya vigezo vya bidhaa au viwango.

Kamati hii ni muhimu katika taasisi ya viwango ambapo husaidia kutoa miongozo juu za bidhaa hafifu, bidhaa hafifu ni zile ambazo hazijakidhi viwango vilivyowekwa na mashirika yaliyothibitishwa ya udhibiti wa viwango vya ubora kitaifa,kikanda na kimataifa .

Bidhaa hafifu huweza kuwa na kasoro, kuwa na malighafi duni, au kuwa na dosari katika utengenezaji. Kamati hii inatoa maana na mantiki ya uwepo wa bidhaa bandia.

i. **Bidhaa bandia:** Hizi ni bidhaa ambazo zimetengenezwa kwa njia ya kughushi au kuiga bidhaa halisi mara nyingi kwa kutumia malighafi ya bei nafuu na duni.

**ii. Bidhaa zilizopitwa na wakati:** Bidhaa

zilizomaliza muda wa matumizi, ambazo bado zipo sokoni zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa afya.

**iii. Bidhaa zenye dosari:** Hizi ni bidhaa ambazo zina mapungufu kwenye muundo au utengenezaji.

**Sababu za kuwa na bidhaa hafifu**

Kwa mujibu wa kanuni,kamati hii imeeleza sababu za kuwa na bidhaa hafifu ni :

**i. Ukosefu wa udhibiti wa ubora:** Nchi au kampuni zinaposhindwa kudhibiti na kufuatilia ubora wa bidhaa zinazoingia sokoni.

**ii. Uelewa mdogo wa matumiaji:** Watumiaji wanaweza kukosa uelewa kuhusu ubora wa bidhaa wanazozinunua na jinsi ya kubaini bidhaa zisizokidhi viwango.

**iii. Ukosefu wa Sheria Madhubuti:** Kukosekana kwa sheria nzuri zinazohakikisha ubora wa bidhaa au utekelezaji dhaifu wa sheria hizo.

**Athari za bidhaa hafifu**

Bidhaa hafifu zinaweza kuwa na athari kubwa kwa afya ya watumiaji na mazingira. Kutokana na udhaifu, bidhaa hizi mara nyingi hazikidhi viwango vya usalama na kwa hivyo kuweza kusababisha madhara ya kiafya, kama magonjwa na majeraha.

Aidha, matumizi ya vifaa hafifu vinaweza kuharibu mazingira. Athari hizi zinaweza kuwa za muda mfupi au mrefu na zinaweza kuathiri sio tu watumiaji binafsi, bali pia jamii na uchumi kwa jumla. Hivyo, ni muhimu kwa wataalamu na wadau kushirikiana ili kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hafifu na kuhakikisha viwango vya ubora vinazingatiwa.

**Njia za kuzuwia bidhaa hafifu**

**i. Kuongeza udhibiti wa ubora sokoni:** Mashirika ya viwango yahakikishe bidhaa zinakaguliwa kabla ya kuwafikia watumiaji.

**ii. Kuongeza uhamasishaji kwa umma:** Kueneza elimu kwa watumiaji kuhusu jinsi ya kutambua na kuripoti bidhaa zisizokidhi viwango.

**iii. Kuweka alama za ubora:** Kuanzisha alama maalum zinazothibitisha kuwa bidhaa imethibitishwa na ina ubora wa kiwango kinachotakiwa.

Mjasiriamali au mzalishaji atahitajika kufuata maelekezo katika uzalishaji wake na kufuata maelekezo, hasa katika kifungashio ambapo taarifa muhimu zitazohitajika kuwekwa katika kifungashio hicho ni kama zifuatazo:-

**i. Jina la bidhaa:** Hii ni taarifa ya msingi inayomsaidia mteja kuitambua bidhaa kwa urahisi.

**ii. Vipengele vya bidhaa (Ingredients):** hivi ni vipengele kwenye bidhaa za chakula na vipodozi vinvyomsaidia mteja kujua vitu vilivyotumika.

**iii. Maelekezo ya matumizi:** Kwa bidhaa kama dawa au vifaa vya umeme, maelekezo ya matumizi ni muhimu ili kuhakikisha matumizi salama.

**iv. Tarehe ya kutengenezwa na kuisha Muda:** Hii ni muhimu hasa kwa bidhaa zinazoweza kuharibika, kama vyakula na dawa.

**v. Maelezo ya lishe (kwa vyakula):** Wateja wanaweza kuona thamani ya lishe wanayopata, kama protini, mafuta na sukari.

**vi. Alama za usalama:** Maelezo au ishara zinazowaongoza watumiaji kuhusu hatari zinazowezekana au hatua za usalama.

**vii. Mahali pa utengenezaji na mtoa huduma:** Maelezo haya yanaweza kumsaidia mtumiaji kuona asili ya bidhaa na kuwasiliana na mtoa huduma iwapo kuna haja hio.

**viii. Jina la Mzalishaji wa bidhaa husika.**

**ix. Namabari ya Kundi (Batch number).**

**x. Kutaja ujazo wa bidhaa.**

**xi. Maelezo ya namna ya kuiharibu bidhaa baada ya matumizi mfano pempasi.**

**xii. Lugha inayotumika katika kuielezea bidhaa.**

**xiii. kutaja daraja ya bidhaa husika kwa bidhaa zenye madaraja.**

**xiv. Kutaja kiasi cha bidhaa za nguo.**

**xv. Kutaja umadhubuti (grammage) kwa bidhaa za vifaa vya karatasi.**

Ni muhimu kwa wazalishaji,wasambazaji na waingizaji wa bidhaa kufuata maelekezo ya kiwango husika katika uzalishaji au uingizaji wa bidhaa ili kuepukana na uingizaji wa bidhaa zilizokuwa chini ya kiwango .

# TARATIBU ZA UKAGUZI WA BIDHAA


1

Muingizaji / wakala atatuma maombi kupitia mfumo wa single window.




2

ZBS atapokea maombi kutoka kwa wakala / muingizaji na kuyachakata



3

ZBS baada ya kuyachakata maombi itatoa kumbukumbu namba ya malipo (control number), ikiwa shehena hiyo haikukaguliwa nje ya nchi au kuwa na Leseni ya Alama ya Ubora ya ZBS/TBS



4

ZBS itafanya ukaguzi na kuchukua sampuli za bidhaa na kuziwasilisha maabara



5

Ikiwa bidhaa imekidhi Viwango mteja atapewa Cheti cha Ubora na kuruhusiwa kuingiza Sokoni.




6

Ikiwa bidhaa haikukidhi Viwango, ZBS itachukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zake.






# ZANZIBAR KUANDAA MKUTANO MKUU WA ARSO, JUNI 2025

**Mkutano Mkuu wa ARSO.**
Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) linatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano mkuu wa Shirika la Viwango la Afrika (ARSO) wa mwaka 2025 .

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa Zanzibar kuwa mwenyeji wa mkutano huu muhimu ambao lengo lake kuu ni kuimarisha viwango na ubora wa bidhaa katika Bara la Afrika.
Katika hatua za kwanza za maandalizi ya mkutano huu , Katibu Mkuu wa ARSO, Dk. Hermogene Nsengimana, alitembelea ofisi za Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) zilizopo Maruhubi, mjini Unguja.

Katiika ziara yake hio alikagua maabara mbalimbali na kuzungumza na uongozi wa ZBS kuhusu maandalizi ya mkutano na kubadilishana mawazo na wenyeji wake.

Dk. Nsengimana alieleza kuridhishwa kwake na maendeleo yaliyofikiwa na ZBS tangu ilipojiunga na ARSO kama mwanachama mwangalizi na kufurahia kuona ongezeko la maabara na mifumo imara ya ukaguzi, ikiwa pamoja na maabara ya uchunguzi wa bidhaa za kemikali zilizopata ithibati ya taasisi ya udhibiti ubora kwa nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika.



**Ushirikiano wa Kitaifa**
Maandalizi ya mkutano huu yanafanyika kwa kushirikiana na Wizara za Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ambazo ndizo zinazosimamia masuala ya viwango. Ushirikiano huu unalenga kuhakikisha

mkutano unafanyika kwa mafanikio na kuleta matokeo chanya katika sekta ya viwango nchini na Afrika kwa ujumla.

Kufanyika kwa mkutano huu Zanzibar kunatoa fursa kubwa kwa Zanzibar kujitangaza kimataifa na kuonyesha uwezo wake katika kusimamia viwango na ubora wa bidhaa.

Mkutano huu utaokuwa na wajumbe wa taasisi za viwango kutoka nchi mbali mbali za Afrika unatarajiwa kuchochea maendeleo ya kiuchumi, kubadilishana mawazo na kuongeza hamasa ya uwekezaji katika sekta mbali mbali.

Vile vile mkutano huu utasaidia kuitangaza Zanzibar katika Nyanja mbali mbali, kama utalii, utamaduni, mila na desturi za watu wake.

Shirika la ARSO ni taasisi ya kanda inayoshughulika na uratibu wa viwango vya bidhaa na huduma katika Bara la Afrika ambayo lilianzishwa ili kusaidia mataifa ya Afrika kuboresha biashara zao, kuhakikisha ubora wa bidhaa, na kulinda walaji dhidi ya bidhaa duni zilizo chini ya viwango.

ARSO ilianzishwa 1977 chini ya mwamvuli wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), ambayo sasa inajulikana kama Umoja wa Afrika (AU). Lengo kuu lilikuwa kuimarisha ushirikiano wa viwango vya biashara baina ya nchi za Afrika na kupunguza vikwazo vya kiufundi kwenye biashara.

**Malengo ya ARSO.**
ARSO inafanya kazi kwa lengo la:-

**i. Kuendeleza viwango vya pamoja vya Afrika:** Kusaidia mataifa wanachama kuwa na viwango vya pamoja ili kurahisisha biashara ya bidhaa.

**iii. Kuhakikisha ubora wa bidhaa**: Kuondoa bidhaa hafifu na hatari kwenye soko la Afrika.

**iv. Kuongeza ushirikiano wa biashara:** Kupunguza vikwazo vya kibiashara vinavyotokana na tofauti za viwango vya bidhaa kati ya mataifa ya Afrika.

**v. Kuhamasisha maendeleo ya viwanda:** Kuboresha uzalishaji wa bidhaa za ndani ili ziwe na ushindani katika soko la kimataifa.

**vi. Kulinda mazingira na afya ya walaji :** Kuhakikisha bidhaa zinakidhi viwango vya usalama na hazina madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

**Mchango wa ARSO katika Biashara na Uchumi.**
ARSO inasaidia nchi za Afrika kupunguza utegemezi wa viwango vya kimataifa kwa kuandaa viwango vinavyolingana na mahitaji ya bara la Afrika. Vile vile inarahisisha biashara kati ya mataifa ya Afrika kwa kuondoa changamoto za utofauti wa viwango na inasaidia biashara ndogo na za kati (SMEs) kupata masoko kwa kuhakikisha bidhaa hizo zinakubalika kimataifa.

**Ushiriki wa ZBS katika ARSO.**
Zanzibar,ikiwakilishwa na ZBS inashiriki katika shughuli za ARSO kama mwananchama muangalizi huku ikipata ushirikiano mzuri wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika kuiwakilisha Tanzania ndani ya ARSO. TBS na ZBS zinahusika na uratibu wa masuala ya viwango nchini na zinashirikiana na wadau mbali mbali katika kuandaa na kutekeleza viwango vya bidhaa na huduma.



# MATUKIO MUHIMU AMBAYO ZBS IMESHIRIKIANA NA ARSO














# TUONAVYO SISI



## SULEIMAN RASHID SEIF

Muazilishi wa bidhaa ya Pemba product

“Napenda kuishukuru ZBS kwa huduma nzuri na msaada mlioutoa katika mchakato wa upatikanaji wa alama ya ubora kwa bidhaa zangu. Utaalamu wenu na ufanisi katika kutekeleza ukaguzi umenisaidia kuimarisha ubora wa bidhaa zangu. Alama hii ya ubora sio tu inachangia kuongeza uaminifu wa wateja, bali pia inafungua milango zaidi katika masoko ya ndani na ya kimataifa.

Nawashukuru kwa kuimarisha viwango vya ubora na kusaidia wajasiriamali, kama mimi kufikia malengo yetu.Nitaendelea kushirikiana nanyi ili kuboresha bidhaa na huduma zetu.Asanteni sana.”



## OMAR HUSSEIN MUSSA

Rais wa Wakala wa Forodha (ZFB)

“Nawashukuru sana ZBS kwa huduma za kitaalamu na ufanisi mlioonyesha katika upatikanji huduma za ukaguzi wa bidhaa bandarini. Huduma zenu zinasaidia kuhakikisha bidhaa zetu zinakidhi viwango vinavyohitajika. Vile vile, mfumo wa sasa umerahisisha uharaka wa kupata huduma. Ujuzi wenu katika ukaguzi na ushirikiano wenu wa karibu umesaidia kufanikisha mchakato huu. Tuendelee kushirikiana.




## TATU SLEIMAN

Mkurugenzi wa Zaidat Product

"Naipongeza ZBS kwa kutoa huduma bora na kwa msaada katika mchakato wa upatikanaji wa alama ya ubora kwa bidhaa zangu.
Huduma yenu imekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha ubora wa bidhaa zangu na kuongeza uaminifu wa wateja. Utaalamu wenu katika ukaguzi na kufanya tathmini umesaidia kufikia viwango vinavyohitajika na kukuza biashara yangu.
Nashukuru kwa ushirikiano wenu wa karibu na msaada wa kitaalamu wakati wa mchakato mzima.Nafasi hii ya kufanya kazi pamoja imeniwezesha kufahamu zaidi kuhusu viwango vya ubora na umuhimu wake katika soko.



## KHAMIS MUSSA KHAMIS

Mdau wa ZBS

Kama wakala wa forodha ninaefanya Ukaguzi wa magari katika taasisi ya ZBS .Huduma hizi zinazotolewa na ZBS ni hatua muhimu kuhakikisha usalama, ubora, na ufanisi wa magari barabarani. Kwani Huduma hii inasaidia kupunguza ajali, kulinda mazingira, na kuhakikisha magari yanakidhi viwango vya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS).

**"Tunawashukuru na tunawakubali ZBS"**

# TUNAJIVUNIA KUWA WACHANGIAJI KATIKA KUFANIKISHA MIRADI YA MAENDELEO YA ZBS



## ASMA ALI MUHSIN

Afisa mipango miradi na takwimu

"Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Taasisi ya Viwango Zanzibar kuthamini uwezo wangu na kuweza kunishirikisha katika uandishi wa miradi mbalimbali mikubwa katika kufanikisha ujenzi wa maabara ya ujenzi hasa katika uaandaji miradi .

Pia shukrani ziende kwa Mkurugenzi Mkuu kwa kutujengea uwezo katika fani zetu. Uwezo huo umechangia kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa mafanikio. Nashukuru na kuahidi kufanya kazi kwa uweledi na ufanisi ili kuweza kufikisha mbele gurudumu la maendeleo ya ZBS"



## SALIM KASSIM JUMA

Afisa Maabara Uhandisi Majengo.

"Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa kushirikishwa kama mtaalamu wa ndani niliyeweza katika kufanikisha miradi mbalimbali ya ujenzi. Ushirikishwaji huu umekuwa wa thamani kubwa katika kuhakikisha ubora na usalama wa miradi yetu na kuboresha utendaji kazi wetu. Ahsante kwa fursa hii na tutaendelea kufanyakazi kwa pamoja ili kuboresha viwango vya ujenzi nchini."




## ENG. SAID JOHN NDEREMA

Afisa Viwango Uhandisi Ujenzi

"Kama mfanyakazi wa ZBS ambaye ni afisa viwango uhandisi ujenzi najivunia kupitia taasisi yangu kunipa ujuzi wa kuniwezesha kitaalamu na kuweza kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ZBS amabyo ili punguza gharama za upatikanaji washauri elekezi kutoka nje. niliupokea mradi wa ujenzi wa maabara ya ugezi ukiwa katika hatua za mwanzo kwa ushirikiano wa mkandarasi, wahandisi na mafundi, umesaidia kutatua changamoto nyingi na kuleta ufanisi. Tunaamini kuwa maabara hii itakuwa na manufaa makubwa kwa maendeleo ya kiufundi na kisayansi katika eneo letu. Tunaushukuru uongozi wa ZBS kwa kutuamini katika ufanikishaji wa miradi hii mikubwa."

# MIRADI YA ZBS







# MATUKIO KATIKA PICHA



Taasisi ya Viwango katika kuhakikisha inatoa uelewa kwa wajasirimali kwa kufanya “Bussiness Forum” Jukwaa la Elimu kwa Wafanyabiashara ikiwa ni njia ya kuwasilisha elimu na maoni kutoka kwa wajasiriamali, Juni 19,2024

Mkurugenzi Usimamizi Ubora kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu ZBS Ndg. Suleiman Abdalla Moh’d akikabidhiana na Mkurugenzi Mtendaji TAHA Ndg. Jacqueline Mkindi cheti cha kukabidhi kifaa Maabara ya Vimelea , Otktoba 19, 2024







ZBS ikishirikiana na ZEEA ilitoa Mafunzo na Zawadi kwa wajasiriamali katika maonesho ya 11 ya biashara ikiwa ni shamra shamra za kuazimisha miaka 61 ya mapinduzi, Januari 8, 2024

Afisa uhusiano na masoko ZBS Ndg. Khadija Rashid Khamis akitoa uelewa juu ya ZBS kwa Watalii walokuja kutembelea Banda la ZBS katika Maonesho ya Utalii, 26 Oktoba, 2024.



# MATUKIO KATIKA PICHA




Katibu Mkuu Wizara ya Biashra na Maendeleo ya Viwanda Mhe. Fatma Mbarouk Khamis na Mkurugenzi Mkuu ZBS Ndg. Yusuph Majid Nassor wakisaini hati ya makabidhiano ya eneo la kujengea maabara za ZBS katika Mtaa wa Viwanda Dunga - Zuze, Agosti 7 , 2024



Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akipanda mnazi katika eneo la kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto katika hafla ya uzinduzi wa kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto Maruhubi - Zanzibar, Agosti 6, 2024



Kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru kitaifa 2024 Ndg. Geodfrey Eliakimu Mnzava akiweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya maabara ya ugezi na kemia katika eneo la Maruhubi - Zanzibar, Mei 18, 2024



Kikao cha bodi ya usimamizi wa kitaalamu wa kamati ya viwango vya Afrika Mashariki kujadili maagizo ya kamati ya usimamizi wa Viwango ambavyo havikufikia makubaliano ya ngazi ya kitaalamu kwa kuunda muongozo utakaosaidia na kuhakikisha kuwa viwango vinavyotumika katika sekta mbalimbali vinakidhi mahitaji na matarajio ya wadau kilichofanyika nchini Kenya, Septemba 5, 2024

# MATUKIO KATIKA PICHA




Hafla ya ufunguzi wa mafunzo na maonesho kwa wadau na watoa huduma katika sekta ya ujenzi ilofanyika katika Hotel ya Golden Tulip - Uwanja wa Ndege - Zanzibar, Disemba 12, 2024

Mkurugenzi Usimamizi Ubora kwa ZBS Ndg. Suleiman Abdalla Moh'd akikabidhi kompyuta 10 za kisasa kwa Rais wa Wakala wa Forodha (ZFB) Ndg. Omar Hussein Mussa katika Mkutano Mkuu wa Wakala wa Forodha , Disemba 28, 2024.





Mhe. Dr. Suleiman S. Jafo Waziri wa Viwanda na Biashara Tanzania akikagua bidhaa ya mjasiriamali yenye alama ya ubora ya ZBS alipotembelea Banda la ZBS katika ufunguzi wa maonesho ya 11 ya biashara ikiwa ni shamra shamra za kuazimisha miaka 61 ya mapinduzi, Januari 5, 2025

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS Ndg. Yusuph Majid Nassor anunua jezi 40 zenye thamani ya shilingi 1,000,000/= , ikiwa ni katika kuiunga mkono Timu ya Taifa ya Zanzibar Heroes, Januari 7, 2025



# MATUKIO KATIKA PICHA



Ziara maalum ya Dr. Khalid Salum Mohammed Waziri wa Ujenzi, Mawasiliana na Uchukuzi katika maabara za kisasa za uhandisi ujenzi za ZBS katika ofisi za makao Makuu ya ZBS - Maruhubi. Februari 24 2025.




Mkurugenzi Mkuu wa ZBS Ndg. Yusuph Majid Nassor na Mkurugenzi Mkuu wa SABS Ndg. Lizo Makele wakitiliana saini ya makubaliano (MOU) nchini Afrika kusini , yenye lengo la kuboresha ubora wa bidhaa na huduma katika maeneo yote mawili. Februari 27,2025




ZBS imetoa msaada wa bidhaa za chakula kwa Jumuiya ya kusaidia watu wenye Mahitaji Maalum kilichopo katika jimbo la Mwakilishi wa jimbo la Mwera Mh. Mihayo Juma Nhunga wenye thamani ya milioni sita (6). Februari 18, 2025.




Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hmed Suleiman Abdulla akimkabidhi tunzo kwa Afisa wa TradeMark Africa (TMA) katika hafla ya uzinduzi wa mfumo jumuishi wa kielectroniki wa ZBS Viwango (iSQMT) iliofanyika katika hoteli ya Golden Tulip. Februari 20,2025.

# WASILIANA NASI

## OFISI KUU

143 MTAA WA TIMBA 71111,
MJINI MAGHARIB,
P.O.Box 1136 ,Maruhubi, Zanzibar
Simu: +255 24 2232225
Faski: +255-24-2232225
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

### OFISI ZINAZOTOA HUDUMA UNGUJA

Bandari ya Malindi, Zanzibar
P.O.Box 1136,
Simu: +255 24 2232225
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

Uwanja Ndege, Zanzibar
P.O.Box 1136,
Simu: +255 24 2232225
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

Bandari ya Fumba, Zanzibar
P.O.Box 1136,
Simu: +255 24 2232225
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

## OFISI PEMBA

PEMBA
KINAZINI CHAKE CHAKE
P.O.Box 352
Simu: +255 24 2452159
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

MKOANI
P.O.Box 352
Simu: +255 24 2452159
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

WESHA CHAKE CHAKE
P.O.Box 352
Simu: +255 24 5244051
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

WETE
P.O.Box 352
Simu: +255 24 5244051
Barua pepe: info@zbs.go.tz
www.zbs.go.tz

Design by: 0718366229

Zanzibar Bureau of Standards

# VIWANGO. UBORA. MAISHA